**RISALA YA UTII YA WANANCHI WA WILAYA YA RUFIJI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DR. JOHN POMBE MAGUFULI KATIKA MAPOKEZI YA MWENGE WA UHURU TAREHE 03/06/2017**

**Mhe.Rais,** Sisi wananchi wa Wilaya ya Rufiji tuna furaha kupata fursa hii ya kuupokea Mwenge wa Uhuru ambao umekuwa chachu ya maendeleo ya Wilaya yetu. Mwenge wa Uhuru umekuwa kichocheo cha maendeleo, uzalendo, umoja, mshikamano na amani ndani ya Taifa letu tangu ulipowashwa na Baba wa Taifa hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere siku ya tarehe 09 Desemba 1961. Wilaya ya Rufiji ina Jumla ya Tarafa **3**, Kata **13**, Vijiji **38** na Vitongoji **177.** Ina ukubwa wa $km^2$ **9,485** ikiwemo hifadhiya Selous yenye jumla ya $km^2$ **6,258**. Ardhi inayofaa kwa kilimo ni $km^2$ 4,824.38 na eneo lenye maji ni $km^2$ **600.** Hifadhi ya Misitu (Misitu ya Serikali kuu, Halmashauri ya Wilaya na Vijiji) ni $Km^2$ **1,656.62.** Idadi ya watu Wilayani Rufiji ni **94,626** wakiwemo wanawake ni **48,943** na wanaume ni **45,683**, hii ni kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka **2012.** Wilaya inapata wastani wa mm.**800** hadi mm.1200 za mvua kwa mwaka. Shughuli kuu ya uchumi kwa watu wa Rufiji ni kilimo. Asilimia **95** ya wakazi ni wakulima, Asilimia **5** ni waajiriwa ofisi za Serikali, mashirika ya umma, sekta binafsi na wengine ni wajasiriamali.

**Mhe.Rais,** kauli mbiu ya mwenge wa uhuru mwaka huu ni "**Shiriki kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi"**. Kwa kuzingatia kaulimbiu hiyo, Wilaya imeweka mikakati ya kukuza uchumi wa viwanda kwa kuanzisha viwanda vikubwa, vya kati na vidogo kwa vitendo. Ili kuwa na viwanda vikubwa, Wilaya imewezesha uandaaji wa eneo katika kata ya Mwaseni lenye ukubwa wa hekta 8,000 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha nafaka na ufuta, Hekta 5,120 kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Sukari na kilimo cha miwa kwenye kata ya Mkongo, Hekta 6,653 kwenye kata ya Chumbi na Hekta 6,600 kwenye kata ya Mbwara kwa ajili ya kilimo cha miwa. Wawekezaji wa kilimo cha miwa katika maeneo hayo wanaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kupata hati miliki katika ngazi ya Wizara. Hata hivyo, Wilaya imewezesha ujenzi wa kiwanda cha kati kwa kushirikiana na mwekezaji mzawa kujenga kiwanda cha maziwa kiitwacho Mother Diary. Matarajio ya ujenzi wa viwanda hivi ni kuongeza ajira na pato la Taifa kwa ujumla. Wilaya ina jumla ya viwanda vidogo 35. Kati ya hivyo viwanda vilivyosajiliwa 8 visivyosajiliwa ni 27. Viwanda hivi vinashughulika na kuongeza thamani kwenye mazao ya maliasili na shughuli zingine za ujasiriamali. Juhudi zingine zilizotekelezwa na Wilaya ni pamoja na kuhamasisha wananchi kushirikiana na wawekezaji ili kuhakikisha kuwa mafanikio hayo yanafikiwa. Wilaya inajitangaza kwa kutumia vyombo vya habari na tovuti ya Halmashauri ya wilaya ya Rufiji kwa ajili ya kuvutia uwekezaji kwenye sekta za kilimo, viwanda na rasilimali za misitu. Wawekezaji wengi wameonyesha nia ya kuja kuwekeza Wilayani Rufiji.

**Mhe.Rais,** katika kuhakikisha kuwa vijana wanafanya kazi zao kwa mafanikio, Wilaya imetenga kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 kiasi cha **Tsh 181,007,600.00** itakayotumika kukopesha vijana na wanawake ambapo jumla ya vikundi 53 vinatarajiwa

kunufaika na mkopo huo. Vikundi 33 ni vya vijana na 20 ni vya wanawake. Kila kijiji kimetenga zaidi ya hekta 10 kwa ajili ya shughuli za vijana.

**Mkakati wa Kupamabana na kuzuia Rushwa.**

**Mhe.Rais**, Wilaya inapambana na vita dhidi ya Rushwa, kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (**TAKUKURU**) inayotekeleza majukumu yaliyoko kwenye Sheria Na. 11 ya mwaka 2007 ya kuzuia na kupambana na Rushwa. Katika kipindi cha mwaka mmoja, taasisi hii imepokea taarifa 117 za vitendo vya rushwa na taarifa zinazohusiana na vitendo vya makosa ya rushwa. Jumla ya wananchi wapatao 7,440 wameelimishwa juu ya madhara ya kujihusisha na vitendo vya Rushwa. Aidha, jumla ya klabu 20 za wanafunzi zimeimarishwa ili kusaidia juhudi za serikali katika kupambana na tatizo la Rushwa.

**Mkakati wa kupambana na dawa za kulevya**

**Mhe.Rais,** Wilaya ya inakupongeza kwa namna unavyolipa uzito tatizo la matumizi ya dawa za kulevya. Wilaya ya Rufiji imeweka mikakati mbalimbali dhidi ya vita ya dawa za kulevya ikiwemo kutoa elimu kuhusu ubaya wa madawa ya kulevya na kuwachukulia hatua za sheria wanaoendelea na matumizi ya dawa za kulevya. Katika kipindi cha Januari 2016 hadi Mei 2017 jumla ya kesi 84 zinazohusiana na dawa za kulevya ziliripotiwa katika kituo cha polisi zikihusisha watuhumiwa 98. Kati ya kesi hizo, 35 zilihusu matumizi ya bangi ambapo jumla ya kg 457.12 zilikamatwa, kesi 5 zilihusu matumizi ya dawa ya "Heroine" ambapo jumla ya gramu 755 zilikamatwa na kesi 44 zilihusu matumizi ya pombe haramu ya gongo, ambapo lita 100.25 zilikamatwa. Jumla ya watuhumiwa 59 kati ya 98 sawa na asilimia 60 walipatikana na hatia. Kati ya hizo, kesi 24 ni za bangi, kesi 3 ni za "heroine" na kesi 32 zilikuwa za pombe haramu ya gongo. Wilaya imefanikiwa kuwezesha vijana 50 waliokuwa wameathirika kwa matumizi ya dawa za kulevya kujiunga na shughuli za uzalishaji mali. Mafanikio haya yamefikiwa kwa ushirikiano kati ya kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya na Jeshi la polisi. Jumla ya ekari 0.75 za bangi ziliteketezwa. Vijana wetu walioelimishwa na kuacha kutumia dawa za kulevya wametushauri kuanzisha SOBA House ili iweze kuwahudumia na kuwapa elimu juu ya madhara na umuhimu wa kuacha kutumia dawa hizo hatari kama mpango endelevu. Wilaya imeomba taasisi ya SOBA house tawi la Bagamoyo kurejesha upya huduma yake katika tawi la Ikwiriri Rufiji.

**Mikakati ya mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI**

**Mhe.Rais,** Wilaya ya Rufiji ina asilimia 5.9 ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Watu wanaoishi na VVU ni 4,235 wakiwemo (Me 1312 na Ke 2923), wanaotumia dawa za kupunguza makali ni 2,023, wakiwemo (Me 558 na Ke 1,465). Katika kupambana na vita dhidi ya VVU, Wilaya imeanzisha Vituo 6 vya kutolea dawa za kapunguza makali ya VVU, vituo 24 vya kutolea huduma ya ushauri nasaha na kupima VVU pamoja na kutoa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Wilaya imetoa elimu kwa watu 20 wakiwemo waganga, wakunga wa jadi na Mangariba kwa lengo la kuwahimiza kuwarudisha wanaoishi na VVU waendelee kupata matibabu hospitalini.

**Mapambano dhidi ya Malaria**

**Mhe.Rais,** Ugonjwa wa malaria ni miongoni mwa magonjwa yanayowasumbua watu wengi wilayani Rufiji. Wastani wa maambukizi ni asilimia 25.2. Mwaka 2015 wagonjwa 37,392 sawa na asilimia 36.5 waliugua malaria, na mwaka 2016 waliougua malaria walikuwa 35,532 sawa na asilimia 24.1. Maambukizi ya malaria kati ya mwaka 2015 na 2016 yalipungua kwa asilimia 12.4 kutokana na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Wilaya. Katika kukabiliana na tatizo hili, wilaya imegawa vyandarua vya kujikinga na mbu wanaoeneza malaria kwenye kaya 23,150. Vilevile, inaendelea kutoa elimu kwenye jamii juu ya kufanya usafi wa mazingira ili kudhibiti mazalia ya mbu wanaoeneza malaria. Pia, Wilaya inagawa dawa za kukinga malaria kwa akina mama wajawazito ambapo wajawazito 1,985 wamegawiwa dawa hizo.

**Mhe. Rais,** Katika kutekeleza ujenzi wa viwanda kwa vitendo, Wilaya imefanikiwa kwa kushirikiana na mwekezaji mzawa kujenga kiwanda cha maziwa kiitwacho Mother Diary. Mradi huu unahamishwa kutoka kwenye jengo la kukodi la mtu binafsi na kuwa na jengo linalomikilikwa na mwekezaji mwenyewe. Mwekezaji huyo anatarajia kuanza uzalishaji kwenye kiwanda kipya mara ujenzi utakapokamilika. Hadi sasa thamani ya mradi ni **Tsh 260,000,000.00**, ambapo kiongozi wa mbio za Mwenge ameweka jiwe la msingi. Faida ya mradi huu ni kujenga afya bora kwa wananchi, ajira, pato kwa mwekezaji na kodi kwa serikali.

**Mhe. Rais,** Wilaya inaendelea kuandaa mazingira mazuri ya kupata huduma za Afya kwa kuboresha kituo cha Afya Ikwiriri baada ya kufanikisha ujenzi wa jengo la upasuaji pamoja na ununuzi wa vifaa tiba ambapo jumla ya Tsh **Tsh 180,000,000.00** zilitumika. Zaidi ya watu 53,000 watanufaika na huduma hii kwa mwaka. Vilevile Mikakati ya ujenzi wa uzio umeanza kwa kufyatua matofali kutokana na harambee iliyoendeshwa na Mkuu wa Wilaya ya Rufiji na kufanikisha upatikanaji wa mifuko 1,000 ya saruji.

**Mhe.Rais,** Wilaya inaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa walimu na wanafunzi ambapo kiongozi wa mbio za mwenge ameweka jiwe la msingi katika ujenzi wa Madarasa mapya 4, Mabweni 2 ya wanafunzi na vyoo matundu 10 na ukarabati mkubwa kwenye ya shule ya Sekondari Utete. Miradi hii inagharimu **Tsh 264,000,000.00.** Sambamba na hilo, Wilaya imejenga shule mpya ya Msingi ya Shaurimoyo iliyoko katika kijiji cha Nyamwage. Jumla ya madarasa 4, Ofisi 1 na vyoo matundu 4 yamejengwa na kukamilika kwa thamani ya **Tsh 69,976,400.00,** kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya na michango ya wawekezaji waliochukua ardhi kwa ajili ya viwanda kwenye kijiji cha Nyamwage. Wilaya inatoa shukrani kwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kwa kuzindua shule hii.

**Mhe Rais**, ili kuondoa tatizo la upatikaji wa maji safi na salama, Wilaya ya Rufiji inaendelea kuboresha mfumo wa upatikanaji wa maji safi na salama katika vijiji vyake. Mwenge wa uhuru umetembelea mradi wa maji Mbwara kama mradi wa mfano ambapo Mradi huu umegharimu **Tsh 217,373,700.00.** Jumla ya watu 4,365 wananufaika na

mradi huu. Aidha, Wilaya inahamasisha wananchi na viongozi mbalimbali kushiriki katika shughuli za kilimo wakiwemo viongozi wa ngazi za juu. Katika kufanikisha hilo kiongozi mmoja ambaye ni Mheshimiwa Diwani Kata ya Mbwara amelima shamba la Ufuta lenye ekari 57 ambalo ndani yake imepandwa miche ya mikorosho ya kisasa 1,180. Wilaya imemwezesha kupata mbegu bora ya ufuta, miche bora ya korosho pamoja na utaalamu, Shamba limegharimu jumla ya **Tshs. 25,000,000.00.** Wilaya inatoa shukrani kwa kiongozi wa mbio za mwenge kutembelea shamba hili.

**Mhe.Rais,** Katika kutekeleza dhana ya Utawala bora, Wilaya imeendelea kujenga ofisi mbalimbali ili kusogeza huduma kwa wananchi. Hii ni pamoja na Ujenzi wa Ofisi za vijiji na kata. Wilaya inatoa shukurani kwa kiongozi wa mbio za mwenge kwa kuweka jiwe la msingi kwenye jengo la Ofisi ya kata ya Chemchem ambapo Ofisi hii itakapokamilika sambamba na zile zingine zitaimarisha suala la maadili na usimamizi wa kudhibiti Rushwa. Mradi huu umegharimu **Tsh 23,000,000.00** hadi sasa ambapo kati ya fedha hizo **Tsh 18,400,000.00** ni mchango wa Halmashauri na **Tsh 4,600,000.00** ni nguvu za wananchi.

**Mhe. Rais,** Wilaya ya Rufiji ina Barabara yenye urefu wa km.840.5, kati ya hizo, barabara za vijiji km.305.10, barabara za Wilaya km.288.4, barabara za Mkoa km.166.0 na barabara kuu km.81.0. Katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kukuza uchumi wa viwanda, mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Rufiji kupitia mfuko wa barabara imefanya matengenezo ya barabara jumla ya km 161.4 kwa thamani ya **Tsh 225,019,759.29**. Hivi sasa Wilaya ina mkakati wa kujenga barabara yenye urefu km 188.75 na ukarabati wa madaraja kwa thamani ya **Tsh 864,960,000.00**. Vilevile Wilaya iko kwenye mchakato wa kuanza ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kilomita 1 katika Mji wa Utete kwa **Tsh.350, 000,000.00.**

**Mhe.Rais,** Wilaya inatambua juhudi za wanawake na vijana katika kushiriki kwenye shughuli za maendeleo. Kikundi cha vijana cha useremala Mkongoni – Ikwiriri ambacho kimetembelewa na mbio za mwenge, Halmashauri ya Wilaya inashirikiana na kikundi hiki kwa kuwapa kazi ya utengenezaji wa madawati ya shule kwa miaka miwili mfululizo (2016 – 2017). Kwa upande mwingine Wilaya imekuwa ikivishirikisha vikundi hivi kwa lengo la kuwasaidia kuboresha hali zao za uchumi na kuwaongezea kipato. Mfano kikundi cha "Lugongwe Construction Group" kimepewa kazi ya ujenzi wa madarasa na mabweni kwenye shule ya Sekondari Utete. Kwa upande wa kikundi cha kinamama, kikundi cha Kimbolembole kilichopo kijiji cha Nyamwage kinachojishughulisha na programu ya **VICOBA** kimefikia hatua ya kukopeshana baada ya kukusanya **Tsh 6,000,000.00** na hivyo kuwasaidia kuendesha biashara ndogondogo na kilimo cha bustani kwa maendeleo yao. Wilaya ya Rufiji imewakopesha Tsh **2, 000,000.00** ili kukidhi maagizo ya Serikali ya kuvikopesha vikundi vya kinamama na vijana. Kikundi hiki kimesharejesha mkopo huo.

**Mhe.Rais,** Katika Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 Halmashauri ilifanikisha mbio hizo kutokana na michango ya wadau mbalimbali ambapo jumla ya Tsh 32,654,000.00 zilikusanywa, kati ya fedha hizo Tsh 2,860,000.00 zilitumika katika kuratibu miradi ya maendeleo sawa na asilimia 9 na fedha zilizobaki zilitumika kufanikisha shughuli zingine za mwenge. Ili kufanikisha mbio za mwenge wa uhuru

mwaka 2017 Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanikisha kupatikana jumla ya **Tsh 44,818,800/=** kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Watumishi wa Serikali | Tsh 6,640,800.00 |
| Kamati ya Ulinzi na Usalama | Tsh 535,000.00 |
| Serikali za Vijiji na Vitongoji | Tsh 543,000.00 |
| Wadau mbalimbali | Tsh 3,100,000.00 |
| Halmashauri ya Wilaya. | Tsh 34,000,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **Tsh 44,818,800.00** |

**Mhe.Rais,** Katika mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 jumla ya miradi 10 yenye thamani ya **Tsh 2,061,922,106.88** ilizinduliwa, kukaguliwa na kuwekewa jiwe la msingi. Miradi hiyo imekamilika kwa asilimia 100. Katika mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu Wilaya ya Rufiji ina jumla ya miradi 9 yenye thamani ya **Tshs. 1,065,507,289.00** ambayo imezinduliwa, kukaguliwa na kuwekewa jiwe la msingi kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| Kiwanda cha maziwa | Tsh 260,000,000.00 |
| Jengo la Upasuaji | Tsh 180,000,000.00 |
| Kikundi cha vijana Mkongoni | Tsh 20,000,000.00 |
| Shule Mpya ya Shaurimoyo | Tsh 69,976,400.00 |
| Mradi wa Maji Mbwara | Tsh 217,373,700.00 |
| Kikundi cha kina mama (VICOBA) | Tsh 6,000,000.00 |
| Shamba la ufuta | Tsh 25,000,000.00 |
| Ofisi ya kata ya Chemchem | Tsh 23,000,000.00 |
| Ujenzi wa Bweni,Madarasa na Vyoo | Tsh 264,157,189.00 |
| **JUMLA KUU** | **Tsh 1,065,507,289.00** |

**Mhe.Rais,** tunatoa wito kwa wananchi wote kuzingatia Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru wa mwaka huu na kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu yake. Ushiriki kikamilifu wa wananchi katika kutekeleza miradi hii utasaidia nchi kuwa na viwanda ili kuongeza pato la taifa kwa ujumla na wananchi kuishi kwa utulivu, amani na upendo, kuepuka UKIMWI, Rushwa, Matumizi ya dawa za kulevya na Malaria. Wananchi wa wilaya ya Rufiji wanakupongeza Kiongozi wa mbio za Mwenge Ndugu **Amour Hamad Amour** na timu yako ya wakimbiza mwenge wote kwa kazi kubwa mnayoifanya. Mungu awabariki sana.

***Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania***
***Ni sisi wananchi wa Wilaya ya Rufiji***

***Imekabidhiwa na:-***

**……………………………………….**
***JUMA ABDALLAH NJWAYO***
***Mkuu wa Wilaya ya Rufiji***
***03.06.2017.***